**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

**KANDA YA DAR ES SALAAM**

**RUFAA YA JINAI NA. 113 YA 2022**

(Kutokana na kesi ya Jinai Na. 355 ya 2021 Mahakama ya Wilaya Kinondoni)

**BAKILI BUSHIRI.....MRIFANI NA.1**

**HERY JUMA.....MRUFANI NA.2**

**SAID HEMED NGOLANIKE.....MRUFANI NA. 3**

**DHIDI YA**

**JAMHURI.....MJIBU RUFAA**

**HUKUMU YA RUFANI**

**S.M. MAGHIMBI, J.:**

Hili ni shauri la jinai kutokana na warufani kutoridhika na maamuzi ya Mahakama ya Wilaya Kinondoni. Warufani walishtakiwa chini ya kifungu Na. 258 (1) na 271 vya sheria ya Kanuni ya adhabu sura ya 16 kama ilivyorekebishwa mwaka 2019.

Mazingira ya shauri hili ni kwamba washtakiwa walishtakiwa kwa kosa la Wizi wa Makarani na Watumishi, ambapo kosa hili liliainishwa na kifungungu kilicho tafsiri wizi. Washtakiwa wote watatu walikana shtaka lililowakabili. Upande wa mashtaka waliita mashahidi 7 na vielelezo 8. Upande wa utetezi walikuwa hawana mashahidi bali washtakiwa wenyewe. Mahakama iliposikiliza pande zote mbili na kuchambua Ushahidi uliotolewa Mahakamani iliwakuta washtakiwa wakiwa na hatia na kisha kuwafunga washtakiwa hao miaka 5 gerezani. Washtakiwa hawakuridhika ndio sababu ya rufaa hii mbele yangu.

Warufani mbele ya Mahakama hii walileta sababu kumi na tatu za rufaa ambazo ni hizi zifuatazo:-

1. Kwamba Mahakama ilijiongoza vibaya kimantiki na kisheria kwa kutumia kielelezo D1 (mikataba ya ajiri) ambacho hakikuingizwa kabisa na kupokelewa mahakamani wakati wa ushahidi.
2. Kwamba Mahakama ilijiongoza vibaya kimantiki na kisheria kwa kutumia vielelezo P1, P2, P3 na P4 kuwatia hatiani wakata rufaa, vielelezo ambavyo maudhui yake hayakusomwa mbele ya Mahakama baada ya kupokelewa kama Ushahidi.
3. Kwamba Mahakama ilijiongoza vibaya kimantiki na kisheria kwa kutumia kielelezo P3 kuwatia hatiani wakata rufaa, kielelezo ambacho wakata rufaa walikubali hasara iliyotokea lakini sio kuhusika na upotevu wa mali na walishinikiziwa kufanya hivyo.
4. Kwamba Mahakama ilijiongoza vibaya kisheria na kimantiki kwa kusema kwamba mkata rufaa namba moja ndiye aliyeandaa karatasi ya kujazia vifaa ambayo iliyotolewa Pamoja na vielelezo P5 na P6 bila uthibitisho wowote kuwa mkata rufaa ndiye aliyeandaa karatasi hiyo.
5. Kwamba Mahakama ilijiongoza vibaya kimantiki na kisheria kwa kuwatia hatiani wakata rufaa kwa kusema kwamba walikuwa ni waajiriwa kwa nafasi ya uangalizi wa godauni (storekeeper) bila kuwepo kwa uthibitisho wa kutosha wa wao kuajiriwa kwenye nafasi hiyo.
6. Kwamba Mahakama ilijiongeza vibaya kimantiki na kisheria kwa kuamua kwamba wakata rufaa ndio walikuwa na wajibu wa kumleta msimamizi wa godauni badala ya upande wa jamhuri kumleta.

7. Kwamba Mahakama ilijiongoza vibaya kimantiki na kisheria kwa kukukataa ushahidi wa wakata rufaa kuwa hawakuwahi kuwa wasimamizi wa godauni na msimamizi wa godauni ni Miraji.
8. Kwamba Mahakama ilijiongoza vibaya kimantiki na kisheria kwa kutozingatia ushahidi wa wakata rufaa kwamba hawakuwahi kuhojiwa waliposhikiliwa kituo cha polisi hivyo haki zao ziliathiriwa.
9. Kwamba Mahakama ilijiongoza vibaya kimantiki na kisheria kwa kutoupa uzito Ushahidi wa warufani kwamba kulikua na matukio ya wateja kuongeza maandishi kwenye risiti za oda, Ushahidi ambao uliungwa mkono na shahidi wa jamhuri;
10. Kwamba Mahakama ilijiongoza vibaya kimantiki na kisheria kwa kuwatia hatiani wakata rufaa kwa kutumia ushahidi wa kimazingira ikiwa haijathibitishwa kuwa walikua waajiriwa kwenye nafasi zao na kulikuwa na mianya mengine ya mali hizo kupotea.
11. Kwamba Mahakama ilijiongoza vibaya kimantiki na kisheria kwa kukubali Ushahidi upande wa mashtaka ambao haukuweza kuthibitisha uwepo na usajili wa kampuni iliyopoteza hivyo vitu.
12. Kwamba Mahakama ilijiongoza vibaya kimantiki na kisheria kwa kuwakuta warufani na hatia na bila kuzingatia kwamba mjibu rufaa hakuweza kuthibitisha kosa hilo kwa kiwango kinachohitajika kisheria.
13. Kwamnba Mahakama ilijiongoza vibaya kisheria kwa kutengeneza hukumu ambayo haikujadili hoja za kisheria,

vipengele vya kosa na haikutaja kosa kisheria vilivyowatia hatiani wakata rufaa.

Warufani waliiomba Mahakama hii kuikubali rufaa hii na kutupilia mbali maamuzi na adhabu iliyotolewa na Mahakama ya Wilaya na hivyo waachililiwe huru.

Mbele ya Mahakama hii wakati wa usikilizwaji, Warufani walikuwa wakiwakilishwa na Bw. Thomas Gahigi waliki msomi na Bw. Mohamed Singano wakili msomi na upande wa wajibu rufaa waliwakilishwa na Bi. Rwetabura Wakili wa Serikali. Mahakama ilitoa amri ya shauri hili kusikilizwa kwa njia ya maandishi na baada ya maandishi kuwakilishwa basi Mahakama iko katika uwezo wa kutoa maamuzi yake.

Warufani katika mawasilisho yao ya maandishi walieleza kuwa katika sababu ya 1 na 5 wanaziunganisha na wanaeleza kutoridhika na maamuzi ya Mahakama ya Wilaya ambayo ilijikita katika kielelezo ambacho hakikupokelewa kama kielelezo ila ilipokelewa kwa utambuzi tu, kielelezo hiko kikiwa ni ID 1. Kielelezo hiki kilikuwa ni kivuli cha mikatabata ya kuthibitisha kuwa washtakiwa wote watatu walikuwa watunza stoo. Na hakimu katika maamuzi yake katika ukurasa wa 5 wa hukumu yake alitumia kielelezo hiko na kueleza kuwa amejiridhisha kuwa warufani walikuwa waajiriwa kwa nafasi ya watunza stoo. Warufani walirejea Kesi ya **Rashid Amiri na Wenzake dhidi ya Jamhuri,** Rufaa Na. 204.2008 Mahakama ya Rufaa. Jaji Lila, alieleza kuwa Ushahidi wowote wa nyaraka uliopokelewa kwa utambuzi na sio kama kielelezo haiwezi kuwa sehemu ya Ushahidi sababu haina thamani ya kuwa Ushahidi.

Katika kutetea sababu ya pili ya rufaa warufani walieleza kuwa katika sababu hii ya pili wanajumuisha na sababu ya 9 ya rufaa.

Wanaeleza juu ya kielelezo P1 ambacho kilipokelewa Mahakamani na kielelezo hicho ni barua za kuomba kazi baada ya kupokelewa maudhi yake haikusomwa na hivyo kuwanyima haki warufani nafasi ya kuuliza maswali. Kiutaratibu kielelezo kinapo pokelewa Mahakamani kinapaswa kusomwa ni takwa la sheria na pia ilikuruhusu maudhui yake kujulikana. Katika hili rejea ya kesi ya **Bulungu Nzungu dhidi ya Jamhuri,** Jinai ya Rufaa No. 39/2018 ilifanywa ilikuwekea msisitizo kwenye mawasilisho ya sababu hii ya rufaa.

Katika sababu ya tatu ya rufaa, Warufani waliwasilisha kuwa mahakama ilikosea kutumia kielelezo P3 kuwatia hatiani warufani kwani kielelezo hicho kilionyesha wao kukubali hasara na sio kukubali upotevu wa mali. Hakimu katika hukumu alionyesha kutumia kielezo hicho katika kutoa maamuzi yake. Katika hili kesi ya Deogratius Kiria dhidi ya Jamhuri, Rufaa ya Jinai Na. 99 ya 2017, inaoyoeleza kuwa kukubali upotevu hakuleti maana ya kukubali wizi.

Katika sababu ya nne ya rufaa, Warufani walieleza kuwa ilielezwa kuwa mrufani namba moja ndiye aliyekuwa akijaza stock sheet ambayo ililetwa Pamoja na ripoti ya upotevu wa mali. Na ilielezwa kuwa stock sheet hiyo ndio iliyo bainisha upotevu wa mali. Stock sheet na ripoti ya upotevu wa mali vilitolewa kama kielelezo P5 na P6. Stock sheet inayoelezwa kujazwa na Mrufani namba moja haina jina wa la sahihi ya mrufaniwa namba 1. Ripoti za upotevu ziliandaliwa na eafanyakazi wa kampuni wanaodai kulikuwa na upotevu hizo zina majina na sahihi za walioandaa. Mashahidi upande wa mashtaka waliohojiwa juu ya hili walieleza kwa Pamoja kuwa stock sheet zilielezwa kuwa zilijazwa na Mrufani namba moja hazina jina lake wala sahihi yake. Kutokana na hili ni wazi kuwa upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha shtaka pasina

shaka kwamba mrufani namba moja ndiye aliyekuwa anajaza stock sheet ambayo ndio inasemekana ni chimbuko la upotevu kubainika.

Kuhusiana na sababu ya 6 na 7 ambazo zilijadiliwa pamoja, warufani walieleza kuwa hakimu katika hukumu alieleza kuwa warufani walikataa kwamba wao sio watunza stoo na kueleza kuwa mtunza stoo alikuwa Miraji, hata hivyo warufani hawakumleta Miraji ili aweze kutoa Ushahidi. Ni kweli warufani walieleza haya lakini lakini kwa uwezo wao wasingeweza kuwa watunza stoo kwa kuwa kazi hiyo ili hitaji kuwa na elimu kubwa kwa sababu ya mali iliyopo, warufani walieleza kuwa wao wana elimu ya darasa la saba.

Aidha Miraji ni mtu ambae alizungumziwa na upande wa Mashtaka kwa mazingira ya kuwa alionekana kazini mwaka 2020 na pia alaiwahi kuonekana akifanya makabidhiano ya vifaa kwa mrufani namba moja lakini hakuna ushahidi thabiti wowote uliotolewa kuthibitisha makabidhiano hayo. Ikiwa upande wa mashtaka walimzungumzia Miraji katia Ushahidi wao. Wao pia walikuwa na jukumu la kumleta Miraji. Kesi ya **Degratius Kiria dhidi ya Jamhuri,** (imetumika hapo awali) ili nukuliwa katika ukurasa wake wa 7. Ambapo Jaji alionyesha umehimu ikiwa katika mazingira kama haya Miraji alipaswa kushtakiwa au upande wa mashtaka kumtimia kama shahidi wao kuthibitisha kesi. Kitendo cha upande wa Jamhuri kushindwa kumleta Miraji katika shauri hili kunaaminisha kuwa warufani hawakuwa watunza stoo.

Sababu ya nane ya rufaa ilijadiliwa kwa minajili kuwa shahidi na 7 askari mpelelezi gladness alieleza Mahakama kuwa yeye ndio alikuwa mpelelezi na kuwa yeye ndiye aliyechukua maelezo ya mrufani namba 1. Na kuwa warufani namba 2 na 3 walichukuliwa maeleze na wapelelezi

wengine. Shahidi huyu aliendelea kueleza kuwa maelezo hayo hakuyaleta mahakamani. Warufani wanaeleza kuwa wao hawakuhojiwa na afande Gladness alikuwa na wajibu wa kuleta maelezo hayo anayo dai aliandika. Na kama walihojiwa basi ni wazi wangeeleza kuhusu Miraji na hivy angekamatwa pia lakini haikuwa hivyo. Kushindwa kuleta maelezo ya warufani kumeathiri haki zao kitendo ambacho ni kinyume na ibara ya 13 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 2002. Polisi kwa mujibu wa sheria walikuwa na wajibu wa kuwahoji lakini hwakufanya hivyo kitendo ambacho wamekiita cha ubaguzi kulingana na matakwa ya sheria.

Sababu ya 9 na ya 10, ziliwasilishwa kwa Pamoja mabapo warufani walieleza kuwa ushahihi ulieleza kuwa kulikuwa na mazingira ya wateja kughushi oda itakayotolewa wakakti wa zoezi la kununua vifaa. Ushahidi huu uliungwa mkono na ushahidi wa upande wa Mashtaka pia kama inavyoonekana katika ukurasa wa 34 wa mwenendo ambapo shahidi na 5 alieleza wazi kuwa wateja walifanya hivyo wakiwa njiani kutoka kwa mtu wa malipo wakielea godauni. Hata hivyo Mahakama pia ilitumia Ushahidi wa mazingira kuwatia hatiani washtakiwa. Ni Dhahiri kuwa kabla ya kutumia Ushahidi wa kimazingira kumtia hatiani mshatkiwa inabidi kutoa kipaumbele na ikague kwa umakini ushahidi wa mazingira mengine alafu ndio ifike kwenye hitimisho. Kwenye kesi hii Mahakama haikufanya hivyo bali ilienda moja kwa moja kwenye kuwatia hatiani warufani kwa Ushahidi wa kimazingira bila hata kuzungumzia mazingira mengine.

Kuwasilisha juu sababu ya rufaa ya 11 warufani walieleza kuwa SM1 alieleza Mahakama kuwa yeye ni mkurugenzi wa Lizy Investment Company ambayo imesajiliwa japo alishindwa kutoa cheti cha usajili juu ya uwepo wa kampuni hiyo. Na warufani wanaeleza kuwa hakukuwa na

uwepo wa kampuni hiyo kilichokuwepo ni Lizy Shop. Kwakuwa hati ya mashtaka inaeleza kuwa mali zilizoibiwa si mali za mtu binafsi bali ni mali za kampuni hivyo kulikuwa na uhitaji wa kuthibitisha uwepo wa kampuni hiyo kitu ambacho upande wa mashtaka ulishindwa kufanya na hivyo kusababisha kushindwa kuthibitisha shtaka kama inavyoonekana kwenye hati ya mashtaka kuwa mali iliyoibiwa ni ya kampuni kwa kutoleta cheti cha usajili.

Sababu ya 12 ilielezwa kuwa, upande wa mashtaka ulishindwa kuthibistisha shtaka kwa kiwango kinachotakiwa kisheria. Ushahidi uliotolewa ulighubikwa na mapungufu kama, kushindwa kuthibitisha kuwa warufani walikuwa watunza stoo kwa kutukuwepo mikataba yao, kushindwa kumleta kama shahidi au mashtakiwa mtu aliyefahamika kwa jina la Miraji Ali. Mtu ambae alikuwa kazini hadi kipindi tukio linatokea na upande wa mashtaka kulijua hili nani jinsi gani warufani waliweza kufanya wizi ikiwa kuna ulizi kuanzia mchana hadi usiku na pia kuna uwepo wa kamera. Kushindwa kuthibitisha haya kunafanya mashtaka dhidi ya warufani kukosa msingi wa kisheria.

Mwisho, katika sababu ya 13 ya rufaa, warufani wameeleza mapungufu yaliyopo katika hukumu ya Mahakama ni mapungufu ambayo hayaku kidhi matakwa ya sheria kama ilivyokatika kifungu cha 312(1) na (2) Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai sura 20 [kama ilivyorejewa mwaka 2022]. Hakimu amewatia hatiani bila kutaja kifungu na pia hakuna mahali Hakimu aliibua viini vya kosa hivyo kupelekea kushindwa kujadili viini hivyo. Haya yamepelekea kukiukwa kwa mahitaji ya lazima katika hukumu kama inavyohitajika chini ya kf. 312 (1). Baada ya kuwasilisha haya warufani waliomba mahakama

ibatilishe maamuzi ya Mahamaka ya Kinondoni na iwaachie huru warufani.

Mjibu rufaa katika kujibu rufaa hii alieleza kuwa atajibu sababu 1,5,6 na 7 kwa Pamoja. Kisha sababu ya 2,3,5,6,9,10,11 na 13 zitajibiwa kila moja.

Katika sababu 1, 5, 6 na 7 zinazohusiana na kama warufani waliajiriwa kama watunza stoo na kutokuwepo kwa Ushahidi kuthibitisha hivyo. Mjibu rufaa alieleza kuwa hakuna ubishani kuwa warufani waliajiriwa kama watunza stoo wa Lizzy Investment Company. Haya Pamoja na nyaraka iliyotolewa na kupokelewa kwa utambuzi, SM1 katika ukurasa wa 8, 13 na 15 alieleza baada ya bidhaa kuibiwa na taarifa hizi kuripotiwa kwake aliwaita wa rufani wote nao walikiri kosa na kuomba msamaha. Barua za kuomba msamaha ambazo ni kielelezo P3 zilitolewa ikiwa ni Pamoja hati ya malipo iliyothibitisha ajira ya warufani katika kampuni tajwa hapo juu. Hata hivyo Ushahidi wa SM 2, SM3, SM5 NA SM 6 wote haw ani waajiriwa wa Lizzy Investment Company na walikiri kuwa warufani ni waajiriwa wenzao na kuwa mrufani namba moja ndio alikuwa mtunza stoo na mrufani namba 2 na 3 walikuwa wasaidizi wake.

Kutokana na Ushahidi wote uliotolewa hakuna namna warufani wanaweza kujiondoa kwenye kosa waliloshtakiwa nalo. Hakuna pia uwezekano wa mashahidi wote wa upande wa mashtaka kueleza ushahidi unao shabihiana ikiwa ni Pamoja na vielelezo vilivyotolewa. Kesi ya **Goodluck Kyando dhidi ya Jamhuri** (2006) TLR 363, Mahakama ilieleza kuwa kila shahidi na ana uzito wake na lazima

aaminiwe na Ushahidi wake ukubalike, isipokuwa kuna sababu za msingi kutokumuamini shahidi. Hivyo sababu tajwa hapo juu hazina mashiko.

Katika sababu ya pili mjibu rufaa alieleza sababu hii haitamchukulia muda wake kwani, kielelezo P2, P3 na P4 vinavyoelezwa havikusomwa mahakamani vilisomwa kama inavyo onekana katika kurasa ya 14 na 21 hata rekodi zinaonyesha kuwa vilisomwa. Hata hivyo kielelezo P1 ambacho kinaelezwa kuwa hakikusomwa bado kina sifa ya kutotupiliwa mbali kwa warufani kwa uwakilishi wa wakili wao wakati wa hoja waliulizwa maswali juu ya barua hizo na yalijibiwa. Hivyo kuonyesha walikuwa na uelewa na maudhui ya kilichoandikwa. Hili linaonyesha kuwa dhumuni la kutaka nyaraka isomwe mahakamani ni ilimaudhui yake ijulikane. Kwa hoja za warufani ilikuwa na wazi wanazijua. Kanuni hii hapo juu ilielezwa katika kesi ya **Chrizant John dhidi ya Jamhuri** Rufaa ya Jinai Na. 313/2015. Hivyo sababu ya pili itupiliwe mbali.

Sababu ya tatu ya rufaa mjibu rufani aliwajibu kwa kueleza kuwa namna gani kielelezo P3 kilipatikana, SM 1 alieleza kuwa baada ya bidhaa kutoonekana. SM1 anaeleza aliwaita washtakiwa wote akawauliza juu ya jambo hilo nao walikubali na kuomba msamaha kwa maandishi na kuomba kuwa hasara hiyo wakatwe kutoka kwenye mishahara yao. Kwa kitendo kinachoelezwa hapo juu kwa warufani kuomba msamaha na kutaka hasara ikatwe katika mishahara yao inaonyesha kuwa warufani walitenda kosa kama walivyoshtakiwa. Hata hivyo, sio kielelezo P3 peke yake kilichotumika

kuwa tia hatiani warufani ni Pamoja na Ushahidi mwingine. Kueleza kuwa walilazimishwa kuandika ni wazo mbadala kwani hakuna mrufani aliyeeleza haya wakati wa utetezi wala kielelezo hicho hakikupingwa wakati kinatolewa kama sehemu ya Ushahidi. Kesi ya Makubi Dogani dhidi ya Jamhuri, Rufaa ya Madai, No. 78/2019 ilieleza kuwa maudhui ya kielelezo kilichopokelewa bila kupingwa ni uthibitisho kuwa yaliyomo yanakubaliwa.

Katika kujibu sababu ya 4 ya rufaa ilielezwa kuwa,Ushahidi unaonyesha kuwa mrufani Na. 1 ndiye aliyekuwa anajaza opening stock ambayo ilipaswa kushabihiana na na ripoti ya SM 3 kuhusu bidhaa zilizopo godauni Ushahidi ambao ni sehemu ya kielelezo P5 kilichopokelewa bila pingamizi. Hii inathibitisha mrufani wa kwanza ni sehemeu yay a upatikanaji wa kielelezo P5. SM PW3 anaeleza alilinganisha opening stock iliyoandikwa na Mrufani Na. 1 na kisha hupeleka ripoti kwa mkaguzi wa hesabu. Ila tarehe 28/2/2020 alihesabu bidhaa na kukuta haziendani na opening stock. Kilichoibua kugundulika kwa utofauti wa bidhaa kwenye stock sheet na uhalisia wa bidhaa ni stock sheet inayotengenezwa na mrufani Na. 1. Hivyo kielelezo P5 kilitokana na taarifa za mrufani namba 1. Hivyo ubashani wake katika sababu ya rufaa namba 4 hauna mashiko.

Katika sababu ya 8 ya rufaa haina mashiko kwani SM 7, WP 4142 D/SGT Gladness alieleza kuwa yeye binafsi alimhoji mrufani Na. 1 alikataa kuiba bidhaa. Na wengine walihojiwa na afisa Polisi wengine na hivyo walihojiwa kituoni.

Mjibu rufaa anaendelea kuwasilisha kwa kuandika kuwa sababu ya 9 nayo haina mashiko kutokana na ushihidi wa SM5 ambae alipohojiwa kuhusu suala la wateja kuongeza bidhaa alikana na kueleza hajawahi shuhudia kitu kama hicho ni uzushi tu. Aidha kama ilivyoelezwa na SM 6 aliandika risiti 2 ya EFD na ile ya kuandika kwa mkono. Hivyo mteja akifika kwa watunza stoo wanalinganisha risiti zote mbili kama zinafana huku akihoji je mtu atawezaje kughushi risiti ya EFD.

Kwenye sababu ya kumi, mjibu rufaa alieleza kuwa haina ubishi kuwa warufani waliajiriwa na SM1 kufanya kazi kama watunza stoo. Waliielekeza Mahakama kwenye Ushahidi wa SM1, SM2, SM3, SM4, SM6 na SM7. Aliendeleak kueleza kuwa kuna hati ya malipo ya wafanyakazi inayothibitisha walilipwa mshahara kila mwisho wa mwezi. SM1 alitoa ushidi pia kuwa mrufani wa pili na watatu ndio walimsaidia mrufani namba 1 kwa kuhakikisha kuwa bidhaa zinatunzwa vizuri na ndio walio kuwa wakitoa bidhaa kilingana na oda za wateja. Mrufani namba 1 ndio alikuwa akitunza funguo za ghala, Ushahidi huu uliunga mkono Ushahidi wa SM5. Ushahidi pia uionyesha hakukuwa na dalili au ishara za uvunjwaji kuingia kwenye ghala, Ushahidi ambao unashabihiana na Ushahidi wa SM7 na kusema kuwa hakuna namna warufani watasema hawakuhusika. Aliendelea kusema kuwa ushahidi huu wakimazingira.Ushaihidi huov unaungwa na kitendo cha wao kuandika andiko la kuomba msamaha ambapo ushahidi huu unapelekea kuonyesha warufani walitenda kosa. Hivyo sababu hii haina mashiko.

Kwenye sababu ya kumi na moja, hii pia ilikuwa sababu nyingine ambayo mjibu rufaa alieleza haina mashiko kwani hakuna lakubishaniwa kwakuwa warufani wote wakati wa utetezi hawakukataa kufanya kazi kwenye kampuni ya SM1 na wakati wa usikilizwaji wa awali haikuwa hoja iliyobishaniwa.

Sababu ya kumi na mbili ilibishaniwa kwa minajili kuwa shtaka dhidi ya warufani lilithibitishwa bila kuacha shaka yoyote. Kwamba warufani wote waliajiriwa na na kampuni SM1 kama watunza stoo, bidhaa zinazodaiwa kuibiwa na wao zilithibitishwa na kielelezo P6, P7 na P5. Hivyo hakuna ushahidi mwingine kuonyesha vingine kuwa warufani hawahusiki na kosa waliloshtakiwa nalo.

Kwenye sababu ya 13 na ya mwisho, mjibu rufaa alieleza kuwa sababu hiyo haitoshi kufanya kilichofanyika kuwa batili ikiwa kuna ujio wa Marekebisho ya sheria. Mapungufu yaliyoelezwa katika sababu hii ya rufaa yanatibika chini ya kifungu 388 cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura ya 20 iliyofanyiwa majerejeo mwaka 2022. Vile vile mjibu rufani alinukuu kesi ya **Mabula Makoye & Amos Shabani dhidi ya Jamhuri, Rufaa ya jinai Na. 277/2017** ambapo suala hilo lilizungumziwa. Kwa hitimisho, Mjibu rufaa aliomba mahakama kuona hatia na adhabu kwa warufani ni halali na rufaa hii kutupiliwa mbali.

Baada ya kupitia mawasilisho ya pande zote mbili, nitazingatia yote yalielezwa katika kuamua rufaa hii. Katika kuamua rufaa hii nitajiongoza kwa kuunganisha baadhi ya sababu za rufaa kutokana na maudhui zake kuhusiana. Kwa kuanza nitaanza na sababu ya 12

ya rufaa ambayo ndani yake itabeba sababu ya 1,2,3,4,5, na ya 7. Sababu ya 12 imejikita kwenye lalamiko kuwa mjibu rufaa hakuweza kuthibitisha kosa kwa kiwango kinachotakiwa kisheria. Ni wazi kuwa ni takwa la kisheria kuwa kabla ya kumtia mshtakiwa hatiani kwa kosa la jinai, kosa hilo lazima liwe limethibitishwa bila kuacha shaka yoyote (angalia kifungu cha 3 (2) (a) cha Sheria ya Ushahidi sura ya 6 kama ilivyorekebishwa 2019). Suala lilipo ni kama wajibu rufaa walitimiza wajibu wao huo.

Katika shauri la rufaa hii warufani wanaona kuwa upande wa mashtaka haukuweza kufikia kiwango cha uthibitisho kama inavyotakiwa. Mjibu rufani alieleza kuwa washtakiwa walikuwa ni waajiriwa kwa nafasi ya watunza stoo katika kampuni ya SM1 na ushahidi juu ya ajira yao uliotolewa. Vielelezo ilikuwa ni mikataba ya ajira ya warufani, lakini kwakuwa vilikuwa ni kivuli vilipingwa na baadae kupokelewa kwa Pamoja kama ID 1(kwa utambuzi tu). Katika mazingira haya chochote kinachopokelewa kwa utambuzi kikawaida si sehemu ya ushahidi kwani hukosa sifa za ushahidi. Haya yalielezwa katika kesi ya **Rashidi Amiri Jaba na Mwenzake dhidi ya Jamhuri, Rufaa ya Jinai No. 204/2008** Mahakama ya Rufaa. Mahakama hii ilieleza kuwa sheria imewekwa wazi kuwa nyaraka halisi au nyaraka ya ushahidi iliyopokelewa kwa utambuzi tu na ambayo haikutolewa kama kielelezo si sehemu ya Ushahidi na haina thamani ya Ushahidi.

Hivyo kwa Mahakama kutumia ID 1 kama sehemu ya Ushahidi ni kweli ilikosea. Pia upande wa mashtaka ulitoa barua ambazo

warufani waliandika kuomba kazi nazo zilipokelewa kama Kielelezo P1, kielelezo hiki pia warufani hawajaridhika kwa kutumiwa na mahakama kwa kueleza kuwa hakikusomwa na kuelezwa mbele ya Mahakama hivyo kukosa sifa za kisheria kutumika kama Ushahidi. Katika kupitia mwenendo wa shauri ni dhahiri kuwa kielelezo P1 hakikusomwa wala kuelezwa mahakamani. Upande wa mrufani walieleza kuwa nia ya kielelezo kusomwa ni ili maudhui yake yajulikane kwa yule ambae kielelezo kina mlenga ajue yaliyomo.

Aidha mjibu rufaa alieleza wakati wa hoja ukipitia mwenendo inaonekakana kuwa warufani walijua yaliyomo katika kilelezo hicho kwani waliweza kujibu hoja kwa ufasaha kama walivyo kuwa wakihojiwa na wakili wao. Katika hoja zinazoelezwa na upande wa mjibu rufaa nimepitia mwenendo na kutokuona mahali warufani wakihojiwa juu ya kielelezo P1. Hivyo kutokusomwa kwake na kutokuonekana kama anavyo sadiki mjibu rufaa, ni kweli kielelezo P1 hakina sifa kutumika na kinaondolewa kama sehemu ya ushahidi. Kukosa sifa kwa kielelezo ambacho hakija somwa kulielezwa katika kesi ya **Karimu Jamary dhidi ya Jamhuri, Rufaa ya Jinai Na. 412/2018**, Mahakama ya Rufaa.

Hata hivyo pamoja na kutokuwepo kwa vielelezo hivyo ambavyo ni mikataba ya ajira na barua za kuomba ajira, bado upande wa mashtaka ulitoa mahakamani hati za malipo ya warufani yote hii ni kwa nia ya kuthibitisha kuwa walikuwa waajiriwa katika Kampuni ya SM1. Katika mwenendo vielelezo P2 vilipokelewa kwa pamoja Mahakamani na kusomwa mbele ya Mahakama. Vielelezo hivi ni

nyaraka zinazoonyesha malipo ya warufani kila mwisho wa mwezi kutoka kwa SM1 kwa utendaji kazi wao hivyo basi ni dhahiri walikuwa wafanyakazi wa hapo na si vibarua kama walivyo jaribu kueleza washtakiwa. Vielelezo hivi vilipokelewa na hapakuwa na pingamizi lolote. Kielelezo kinachopokelewa bila kupingwa kisheria ni kwamba kimekubalika, haya yameelezwa katika kesi ya **Makubi Digani dhidi ya Ndodongo Maganga, Rufaa ya Madai Na. 78/2019**, ambapo Mahakama ilieleza kuwa maudhi ya kielelezo ambacho kimepokelewa bila kupingwa ni dhahiri yamethibitishwa kwa kutokuwepo pingamizi.

Hivyo kwa upande wa wajibu rufani, waliweza kuthibitisha warufani kuwa waajiriwa wa kampuni ya SM1 kupitia kielelezo P2. Aidha baada ya washtakiwa kuthibitika kuwa waajiriwa wa ofisi inayo washtaki vipo vielelezo vilivyotumika kuwatia hatiani. Zipo barua ambazo zinaonyesha washtakiwa wote watatu waliandika kukiri upotevu wa mali katika ghala la kazini. Kwa muonekano wa barua washtakiwa hawakukiri wizi katika barua hizo bali walikiri upotevu wa mali ambazo ni bidhaa zilizokuwepo katika sehemu yao ya kazi.

Shtaka waliloshtakiwa nalo ni wizi ambapo kwa barua hizi haiwezi kuthibitisha kuwa waliiba vifaa hivyo kwani viini vya kosa la wizi na kukubali upotevu hutofautiana. Viini ambavyo vingethibitisha upotevu wa bidhaa ni uzembe. Na kwa kupitia mwenendo ni wazi kuwa washtakiwa hawakubishania barua hizi kwani inaonyesha waliamini kuwa kilichotokea ni upotevu na si wizi ndio maana walikubali kukatwa gharama na muajiri wao na SM1 alikuwa tayari kwa hilo, kwasababu hiyo barua hizo hazitapewa uzito.

Aidha katika mwenendo kuna kielelzo P5 ambacho kinaonyesha mapokezi ya vifaa na P7 ambacho ni ripoti ya uhakiki wa bidhaa. Vielelezo hivyo vinathibitisha kutolewa kwa bidhaa hizo. Vilevile kulikuwa na ushahidi mwingine wa SM1, SM 4 na SM 5 ambao ulikuwa na mashiko kwakuwa ulishabihiana na mashahidi wengine upande wa Mashtaka ambao walionyesha kuwatambua warufani kama wafanyakazi wenzao waliokuwa wanahusika na stoo.

Warufani kwa ujumla wao walikana kuwa waajiriwa na kueleza kuwa vibarua. Nimepitia utetezi wao kwa makini sana na kutoona uthibitisho wowote wa wao kuwa vibarua na wala hawakutoa uthibitisho wa kuwa vibarua. Katika kielelezo P2 ni wazi kuwa warufani walilipwa mishahara kila mwisho wa mwezi, walikuwa na sifa ya kukopa, walikuwa wanachama wa NSSF na wachangiaji pia, walikatwa pia kodi ya mshahara. Mambo yote haya ndani ya kielelezo P2 kunafanya warufani kupoteza sifa kuwa vibarua na pia kwa kuzingatia kuwa hakuwahi kunaka kuwa wapokeaji mishahara kama kielelezo P2 kinavyoonyesha.

Mazingira ya shauri hili na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka ni dhahiri unaonyesha kuwa mshtakiwa Na. 1 ndio alikuwa mtunza stoo na ndiye aliyekuwa mpokeaji wa vifaa vinapoingia ghalani na ndiye alikuwa muidhinishaji wa vifaa vya kutoka stoo baada ya mteja kuja na mahitaji yake kutoka ofisi ya mhasibu. Haya yalielezwa na mashahidi wa upande wa mashtaka na vilevile mashahidi hao waliongeza kuwa mshtakiwa Na. 2 na 3 hawakuhusika na kuidhinisha vifaa kutoka godown wala kuandika ripoti. Wao kazi

yao kama wasaidizi wa Mshtakiwa Na. 1 ilikuwa kupokea oda kutoka kwa Mashtakiwa Na. 1 na kisha kutoa mzigo ambao mshtakiwa anatoa maelezo utoke. Kwa mazingira ya ushahidi juu ya Mshtakiwa Na. 2 & 3, haionyeshi kama walikuwa na uwezo au nafasi ya kumkagua mshtakiwa Na. 1 kwa oda alizo wajulisha kutoa kwa mteja wala kukaguwa ripoti alizoaanda kwani kama mkaguzi alikuwa ni mtu mwingine.

Katika mazingira hayo kwakuwa oda zilikuwa zikitokea kwa muhasibu kuja moja kwa moja kwenda kwa mshtakiwa Na. 1 ambae aliidhinisha sasa oda ya kutolewa ghalani, ni vigumu kuwaona kuwa washtakiwa Na. 2 na 3 walihuska kwa wizi uliotokea kwani kazi yao ilikuwa ni kutoa mzigo tu. Hivyo ni wazi kusema kuwa mahakama ilikosea kisheria kuona kuwa washtakiwa Na. 2 na 3 walihusika kwa namna moja au nyingine na wizi huo hivyo kuwatia hatiani kimakosa.

Katika kuangalia sababu ya 6 ya rufaa, warufani hawakuridhika na Mahakama kuona kuwa wao ndio walikuwa na jukumu la kumleta msimamizi wa ghala badala ya mjibu rufaa. Walieleza kuwa kuna wakati mtunza stoo alikuwa ni Bw. Miraji Ali na ameongelewa na hata na SM2 kuwa tarehe 30/05/2021 alishuhudiwa akifanya makabidhiano. Mjibu rufaa pamoja na kulinganisha sababu hii ya sita na sababu ya 1,5,6, na ya 7 hakuzungumzia kabisa juu ya sababu hii hivyo basi sababu hii haitachukua muda wangu mwingi. Ni wazi katika misingi ya sheria kuwa kuita mashahidi au kushtaki mtu kunategemea na ushahidi uliopo. Ikiwa Upande wa wajibu rufaa waliona uhusika wa Bw. Miraji ni muhimu basi wangekuwa na uwezo

wa kumleta kwa nafasi amabyo waliona inafaa. Mahakama iliona kuwa wajibu rufaa ndio walipaswa kumleta kutokana na wao kueleza kuwa Bw. Miraji ndio alikuwa mtunza stoo. Hivyo wajibu rufani walikuwa katika nafasi ya kumuita kama shahidi au huenda wangeomba aongezwe kama mshtakiwa. Hata hivyo kwa mahakama iliyotoa maamuzi sioni kwa namna yoyote kama iliingiliana na kusababisha wao kukosa haki yao kwa namna yoyote ile kwani kutomwita kwako hakujafanya shaka dhidi ya ushahidi wa wajibu rufani. Hivyo basi sababu hii haina mashiko.

Katika sababu ya 8 ya rufaa warufani hawakuridhika na kitendo cha kutohojiwa pale walipokuwa wamekamatwa na kuwa kituo cha polisi hivyo kuona kuwa haki zao ziliathiriwa. Upande wa mrufani hawakupoteza muda kwenye hili walieleza kuwa SM 7 ambaye ni mpelelezi alishalitolea hili ushahidi kuwa yeye aliandika maelezo ya mrufani namba 1 na wengine waliandikwa na askari wengine. Hoja ya kwamba kama waliandikwa maelezo mbona hayakutolewa mbele ya mahakama si ya msingi kwani mwenye kuona ni ushahidi gani alete ni muendesha mashtaka, ali mradi atimize wajibu wake wa kuthibitisha kosa juu ya shaka lolote. Hivyo naona hoja hii haina mashiko. Ni kweli sheria inaelekeza mtuhumiwa kuchuliwa maelezo punde tu anapokamatwa lakini sheria hailazimishi maelezo hayo kutumika kama sehemu ya ushahidi. Washtakiwa walikuwa na haki ya kutaka maelezo yao yatolewa kama sehemu ya ushahidi wao kutoka kwa upande wa wajibu rufaa lakini hawakufanya hivyo. Hivyo sababu hii hainamashiko pia.

Kuhusiana na sababu ya 9 ya rufaa, ubishani ni juu ya warufani kutoridhishwa na ushahidi wao kutotumika pale walipoeleza kuwa wateja huwa na tabia ya kubadili idadi ya vifaa wanapokuwa njiani kutoka kwa mlipwa fedha kuelekea stoo. Hili lilipingwa na mjibu rufaa kwa kueleza kuwa risiti hutolewa mbili ya kuandikwa kwa mkono na ile ya kielektoroniki hivyo mtu wa stoo hulinganisha hizo mbili kabla ya kutoa mzigo. Katika ushahidi PW 6 ambae ni mpokea fedha na mhasibu alieleza Mahakama kuwa katika utendaji wao hutoa risiti ya kuandika kwa mkono na ile ya kielektroniki hivyo na risiti hizi hutumika katika kuangalia usahihi wa bidhaa pale mteja anapofika stoo ambapo anawakuta warufani ambao ndio wanatoa mzigo. Na pia hakuwahi kukutana na mazingira yanayo elezwa na warufani. Warufani walikuwa na wajibu huo bali hawaonekani kutenda matakwa hayo yakisheria. Shahidi huyu Na. 6 katika kuthibitisha haya alitoa risiti ambazo zilipokelewa kama vielelezo na kusomwa. Kwa ushaidi huu uliotolewa ni dhahiri kuwa Ushahidi wa PW6 ulikuwa na mashiko hivyo kupelekea mahakama kuamua kwa namna ilivyoamua. Kwa haya ni wazi sababu hii haina uzito kisheria.

Sababu ya 10 ya rufaa imebishaniwa kuwa ushahidi uliotumiwa na mahakama kuwatia hatiani warufani kwa kile Mahakama ilichoeleza ni ushahidi wa kimazingira. Upande wa warufani hawakuridhika na ushahidi huo wakimazingira wakati upande wamjibu rufaa uliunga mkono Mahakama kwa uamuzi wa kutumia ushahidi huo. Katika hili ni wazi kuwa Mahakama ilitumia ushahidi wa kimazingira kuwatia hatiani warufani. Ushahidi huu wakimazingira

tayari umeshaelezwa katika kesi mbalimbali kuwa ni lazima ionekane kuwa hakuna njia wala namna yoyote inayoweza kutiliwa shaka ila ushahidi uelekeze kuwa ni washtakiwa tu na si mtu mwingine ambae angeweza kutenda kosa linalomkabili. Hii ndio kanuni ambayo kabla hujatumia ushahidi wa kimazingira lazima Mahakama ijiridhishe. Kesi ya **Mpunzu@ Elisha Mpunzu dhidi ya Jamhuri (Rufaa ya Jinai No.12 ya 2002) [2004] TZCA 3(28 June 2004),** ilielezea vizuri kanuni ya ushahidi wa kimazingira ambayo na mimi naisisitiza na kuiunga mkono.

Ushahidi uliopo unaeleza warufani ndio watu waliokuwa wahusika na ndio walikuwa wanatunza stoo na kufanya kazi ya kupokea vifaa vinapoingia na kuvitoa kwa wateja vinapotoka. Hata hivyo ushahidi wa upande wa mashtaka uliendelea kuonyesha kuwa ni mrufani namba 1 ambae alikuwa mtunza stoo na funguo alikuwa anakaa nazo yeye. Warufani Namba 2 na 3 walikuwa wasaidizi wake na wote walihusika kupokea na kutoa mizigo kwa amri ya Muomba Rufa Na. 1, hivyo hakuna namna mtu mwingine angeweza kuhusika na utoaji wa mizigo hiyo isipokuwa wao. Lakini kutokana na kuwa Mrufani Na. 2 na 3 walikuwa wakifuatisha maelekezo ya mkubwa wao Mrufani Na. 1, ushahidi huu wa mazingira uliotumika unawaondoa mshatkiwa Na. 2 na 3 kuwa sehemu ya wizi kwani hawakuwa na jukumu la kupakuwa, kuidhinisha wala kutoa vifaa katika godown ambapo vifaa vilitunza ila kwa maelekezo ya Mrufani Na. 1. Mwenye jukumu hilo alikuwa Mshtakiwa na 1 na anabanwa na ushahidi huu wa kimazingira. Hivyo basi naungana na kilichoamuliwa

na Mahakama ya Kinondoni, kwa upande wa Mshtakiwa Na.1 ushahidi ulithibitika juu yake dhidi ya kosa alilotiwa nalo hatiani.

Katika sababu ya 11 usajili na uwepo wa kampuni inayoelezwa kupoteza vitu ndio ilikuwa imebishaniwa. Warufani hawakuridhika na Ushahidi wa upande wa mashtaka kwa upande huo. Ushahidi wao ulikana kuwa walikuwa wameajiriwa na kampuni bali walieleza kuajiriwa na Elizabeth Mtei. SM1 yeye na mashahidi wa upande wa mashtaka walitoa Ushahidi wakieleza juu Lizzy Investment Company, hivyo ni dhahiri kampuni ilikuwepo. Na SM1 alieleza kwanza ilikuwa ni Lizzy Shop kisha baadae ikasijiliwa kuwa kampuni. Hata hivyo suala la usajili halikuwa suala linalobishaniwa kwani warufani walikubali kuwa wameajiriwa na Lizzy Investment Co. Ltd inayomilikiwa na Elizabeth Mtei. Suala la kubishaniwa ni wizi kosa ambalo warufani walishtakiwa nalo. Sababu hii naiona ni hoja dhania iliyojitokeza baadae katika harakati za warufani kujaribu kujinasua katika hatia waliyokutwa nayo.

Mwisho kabisa katika sababu ya 13, warufani hawakuridhika na namna Mahakama ilivyo andika hukumu kwani haikujadili hoja za kisheria, vipengele vya kosa na haikutaja kosa na sheria vilivyowatia hatiani wakata rufaa. Hakimu aliwatia hatiani warufani bila kutaja kifungu kilichovunjwa wala sheria iliyovunjwa huo ni uvunjifu wa kf cha 312 (2) cha sheria ya Mwenendo wa Jinai. Hata hivyo hukumu hiyo haikuwa na mahali palipoonyesha viini vya kosa na havikujadiliwa.

Kifungu cha 312 (1) cha Sura ya 20, kinaeleza juu ya maudhui ya hukumu. Kifungu hiki kinaeleza kuwa hukumu lazima iwe na viini vya kufanyiwa maamuzi, uamuzi utokanao na viini na sababu za maamuzi. Vilevile itakuwa na tarehe na itasainiwa na hakimu kwa tarehe iliyosomwa. Kwa kupitia hukumu iliyotolewa na hakimu aliyesikiliza shauri lililowakabili warufani matakwa yote tajwa hapo juu yanajidhihirisha katika hukumu hiyo. Hakimu aliibua kiini ambacho nanukuu *"whether the prosecution has succeeded to prove their charges and beyond reasonable doubt".* Hivyo warufani walijipotosha kufikiri kiini cha kosa hakikuibuliwa katika hukumu hiyo. Aidha katika ukurasa wa 9 sikubaliani na warufani kuwa Mahakama haikuwatia hatiani kwani mahakama ilihitimisha:

*"in the upshot of the above this court finds the accused persons guilty of the offence of stealing by servant and therefore proceeds to convict them as charged"*

Kwa rekodi hapo juu Mahakama iliwatia hatiani washtakiwa kwa kosa waliloshtakiwa nalo hivyo hakuna mapungufu kama inavyodaiwa. Kutokana na yote yaliyoelezwa na kuamuliwa hapo juu, mahakama hii inakubali sehemu ya rufaa. Kutiwa hatiani kwa Mrufani Na. 2 na 3 hakukuwa sahihi kutokana na mapungufu ya Ushahidi wake. Hivyo basi Mahakama inawaacha huru warufani Na. 2 na Na. 3 labda kama atakuwa wanashikiliwa kwa makosa mengine.

Kwa upande mwingine rufaa ya mshtakiwa Na. 1 haina mashiko yoyote kwani Ushahidi dhidi yake umeweza kuthibitishwa kwa kiwango kinachopswa, pasina shaka yoyote. Mahakama hii haijaona

mapungufu yoyote kuisababisha kuingilia maamuzi ya Mahakama ya wilaya Kinondoni, hivyo basi rufaa hiyo inatupiliwa mbali.

Imesomwa Dares Salaam leo tarehe 15 Agosti, 2023.

THE HIGH COURT OF TANZANIA

.....

**S. M. MAGHIMBI**

**JAJI**